TANGAZO LA SERIKALI Na. 146 la tarehe 28/2/2025

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 14(1))*

AMRI YA KUTANGAZA ENEO LA PORI LA AKIBA MKUNGUNERO YA MWAKA 2025

KWA KUWA, mnamo mwaka 1996 Pori la Akiba Mkungunero lilipandishwa hadhi kutoka pori tengefu na kuwa Pori la Akiba Mkungunero kwa Tangazo la Serikali Namba 307 la Mwaka 1996, chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 1974, likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 743;

NA KWA KUWA, kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283 kinampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa Pori la Akiba;

NA KWA KUWA, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na baada ya kushauriwa ipasavyo, ameridhia kufanyika kwa marekebisho ya mpaka wa Pori la Akiba Mkungunero kwa kupunguza ukubwa wa eneo kutoka kilometa za mraba 743 hadi kilomita za mraba 597 natayari marekebisho hayo yamekwishafanyika;

HIVYO BASI, Mimi, SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori natangaza kama ifuatavyo:

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Eneo la Pori la Akiba Mkungunero ya Mwaka 2025.

Kutangaza pori la akiba

Sura ya 283

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Pori la Akiba Mkungunero kwa mujibu na kwa madhumuni ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

*Tangazo la Serikali Na.146 (Linaendelea.)*

Kufutwa TS. Na. 307 la 1996

**3**. Amri ya Kutangaza Eneo la Pori la Akiba Mkungunero ya Mwaka 1996, inafutwa.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

PORI LA AKIBA MKUNGUNERO

| NAMBA YA KIGINGI | UELEKEO | UMBALI (M) | KASKAZINI | MASHARIKI |
|---|---|---|---|---|
| EAX395 (kusini magharibi mwa Hifadhi ya Taifa Tarangire) Alama ya kuanzia | | | 9494701.407N | 175946.811E |
| | 89°56'30.38" | 19247.021 | | |
| EAX406 | | | 9494720.967N | 195193.823E |
| | 159°56'06.75" | 1312.69 | | |
| EAX406A | | | 9493487.948N | 195644.185E |
| | 82°29'13.60" | 3757.29 | | |
| MGR1 | | | 9493979.210N | 199369.215E |
| | 161°49'31" | 16070.99 | | |
| MGR2 | | | 9478710.000N | 204382.000E |
| | 179°19'10.94" | 16935.94 | | |
| MGR3 | | | 9461587.852N | 204494.107E |
| | 272°59'32.34" | 8886.03 | | |
| MGR4 | | | 9462051.721N | 195620.190E |
| | 338°13'03.63" | 15829.43 | | |
| MGR5 | | | 9476750.937N | 189746.182E |
| | 268°38'43.16" | 10601.40 | | |
| MGR6 | | | 9476500.305N | 179147.743E |
| | 8°39'41.62" | 1820.86 | | |
| MGR7 | | | 9478300.402N | 179421.961E |
| | 56°26'32.43" | 901.12 | | |

*Tangazo la Serikali Na.146 (Linaendelea.)*


| NAMBA YA KIGINGI | UELEKEO | UMBALI (M) | KASKAZINI | MASHARIKI |
|---|---|---|---|---|
| MGR8 | | | 9478798.518N | 180172.889E |
| | 351°50'48.07" | 914.08 | | |
| MGR9 | | | 9479703.357N | 180043.252E |
| | 329°09'22.98" | 1162.89 | | |
| MGR10 | | | 9480701.777N | 179447.044E |
| | 343°05'33.03" | 1044.66 | | |
| MGR11 | | | 9481701.284N | 179143.227E |
| | 2°59'45.26" | 2001.18 | | |
| MGR24 | | | 9483699.724N | 179247.818E |
| | 8°28'33.49" | 2022.94 | | |
| MGR25 | | | 9485700.566N | 179545.988E |
| | 323°02'36.24" | 2500.78 | | |
| MGR26 | | | 9487698.916N | 178042.495E |
| | 339°53'24.81" | 1065.47 | | |
| MGR27 | | | 9488699.427N | 177676.167E |
| | 335°08'23.73" | 865.91 | | |
| VD63 | | | 9489485.099N | 177312.135E |
| | 338°52'00.59" | 1303.74 | | |
| MGR28 | | | 9490701.185N | 176842.160E |
| | 349°32'45.61" | 2034.93 | | |
| MGR29 | | | 9492702.333N | 176472.931E |
| | 7°02'15.98" | 1004.75 | | |
| MGR30 | | | 9493699.514N | 176596.036E |
| | 327°03'24.59" | 1193.85 | | |
| EAX395 (kusini magharibi mwa Hifadhi ya Taifa Tarangire) Alama ya kuanzia | | | | |

PORI LA AKIBA MKUNGUNERO

MAELEZO YA MPAKA WA ENEO

Kipande chote cha Ardhi ya eneo lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 597 kilichopo katika Wilaya ya Kondoa katika Mkoa wa Dodoma kama kilivyoainishwa kweye Ramani ya upimaji yenye usajili Na. 182023 kimeelezwa kijiografia kama ifuatavyo:

Kuanzia kwenye kigingi kilichopo kusini magharibi mwa Hifadhi ya Taifa Tarangire Na. EAX395 (9494701.407N, 175946.811E), mpaka utaelekea mashariki kwa umbali wa mita 19247.021 hadi kigingi kilichopo kusini mashariki mwa Hifadhi ya Taifa Tarangire EAX406 (9494720.967N, 195193.823E), kisha mpaka utaelekea kusini mashariki kwa umbali wa mita 1312.69 hadi kigingi Na. EAX406A (9493487.948N, 195644.185E), kisha mpaka utafuata uelekeo wa mashariki kwa umbali wa mita 3757.29 hadi kigingi Na. MGR1 (9493979.210N, 199369.215E) kisha mpaka utaelekea kusini mashariki kwa umbali wa mita 16070.99 hadi kigingi Na. MGR2 (9478710.000N, 204382.000E) kilichopo mpakani mwa Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara, kisha mpaka utaelekea kusini kufuata mpaka wa Mkoa wa Dodoma na Manyara kwa umbali wa mita 16935.94 hadi kigingi Na. MGR3 (9461587.852N, 204494.107) kisha mpaka utaelekea magharibi kwa umbali wa mita 8886.03 hadi kigingi Na. MGR4 (9462051.721N, 195620.190E), kisha mpaka utaelekea kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 15829.43 hadi kigingi Na. MGR5 (9476750.937N, 189746.182E), kisha mpaka utaelekea magharibi kwa umbali wa mita 10601.40 hadi kigingi Na. MGR6 (9476500.305N, 179147.743E), kisha mpaka utafuata uelekeo wa kaskazini kwa umbali wa mita 1820.86 hadi kigingi Na. MGR7 (9478300.402N, 179421.961E) kisha mpaka utaelekea kaskazini mashariki kwa umbali wa mita 901.12 hadi kigingi Na. MGR8 (9478798.518N, 180172.889E) kisha mpaka utaelekea kaskazini kwa umbali wa mita 914.08 hadi kigingi Na. MGR9 (9479703.357N, 180043.252E) kisha mpaka utaelekea kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 1162.89 hadi kigingi Na. MGR10 (9480701.777N, 179447.044E) kisha mpaka utafuata uelekeo huo wa kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 1044.66 hadi kigingi Na. MGR11 (9481701.284N, 179143.227E) kisha mpaka utafuata uelekeo wa kaskazini kwa umbali wa mita 2001.18 hadi kigingi Na. MGR24 (9483699.724N, 179247.818E) kisha mpaka utafuata uelekeo wa kaskazini mashariki kwa umbali wa mita 2022.94 hadi kigingi Na. MGR25 (9485700.566N, 179545.988E) kisha mpaka utaelekea kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 2500.78 hadi kigingi Na. MGR26 (9487698.916N, 178042.495E), kisha mpaka utafuata uelekeo huo wa kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 1065.47 hadi kigingi Na. MGR27 (9488699.427N, 177676.167E) kisha mpaka utafuata uelekeo huo kwa umbali wa mita 865.91 hadi kigingi Na. VD63 (9489485.099N, 177312.135E) kisha mpaka utafuata uelekeo huo kwa umbali wa mita 1303.74 hadi kigingi Na. MGR28 (9490701.185N, 176842.160E), kisha mpaka utafuata uelekeo huo wa kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 2034.93 hadi kigingi Na. MGR29 (9492702.333N, 176472.931E) kisha mpaka utaelekea kaskazini mashariki kwa umbali wa mita 1004.75 hadi kigingi Na. MGR30 (9493699.514N, 176596.036E) kisha mpaka utaelekea kaskazini magharibi kwa umbali wa mita 1193.85 hadi kigingi Na. EAX395 kilichopo kusini magharibi mwa Hifadhi ya Taifa Tarangire alama ya kuanzia.




Amri hii imeshuhudiwa kwa saini yangu na kuwekwa Lakiri ya Umma leo tarehe 7 Februari, 2025

L.S

IKULU,
Dodoma,

SAMIA SULUHU HASSAN,
*Rais*